**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE**


**SHULE YA SEKONDARI ILEMBULA,**
**S.L.P 33,**
**ILEMBULA.**

**SIMU NA: 0755564572 (MKUU WA SHULE)**
**0753721679 (MAKAMU M/SHULE)**
**0753702688 (MWALIMU WA TAALUMA)**


JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILEMBULA WILAYA YA WANGING'OMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninayofuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 shule ya sekondari Ilembula ipo Halmashauri ya wilaya ya wanging'ombe. Muhula wa kwanza masomo utaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/01/2021 ndani ya siku saba.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 Mahitaji ya sare za shule

## A. WASICHANA

- Suruali mbili (2) bluu nyeusi na damu yam zee, gauni mbili (2) nyeupe mikono mirefu (kisoro chenye marinda) mshono wa gauni umeambatanishwa kwenye form hii.
- Sweta la kijani.
- Jozi mbili (2) za viatu vyeusi vyenye kamba visivyo na visigino virefu (yeboyebo haziruhusiwi kabisa)
- Soksi nyeupe jozi mbili
- Nguo za ndani za kutosha.
- Sare za michezo track suti nyeusi, raba nyeusi na taulo.

## B. WAVULANA

- Suruali mbili (2) bluu nyeusi na damu yam zee.
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
- Sweta la kijani
- Jozi mbili (2) za viatu vyeusi vyenye kamba visivyo na visigino virefu (yeboyebo haziruhusiwi kabisa)
- Soksi nyeusi.
- Nguo za ndani za kutosha

- Sare za michezo track suti nyeusi, raba nyeusi na taulo.

## MAHITAJI MENGINE

- Mwanafunzi aje na bunda moja la karatasi (RIM) ya A4
- Faili moja la kutunzia kumbukumbu binafsi za mwanafunzi
- Wazazi/ walezi wa wanafunzi wa kike wanatakiwa kuchangia Tsh:2000/= kwaajili ya upimaji wa mimba kwa mwaka mzima.

## 3.0. MAHITAJI YA HOSTELI

## A. WANAFUNZI WANAOKAA HOSTELI

i. Mahindi debe kumi (10) kwa mwaka
ii. Maharage debe mbili (2) kwa mwaka
iii. Mchele debe moja (1) kwa mwaka
iv. Sukari kilo nne (4) kwa mwaka
v. Fedha Tsh:140,000/= (laki moja na arobaini)
vi. Godoro la futi mbili na nusu (futi 2 ½ )
vii. Mashuka mawili rangi ya pink na blanketi
viii. Sahani, kijiko na kikombe.
ix. Vifaa vya usafi binafsi (ndoo 1 ya ujazo wa lita kumi, kiwi, taulo, mswaki, dawa ya mswaki, mafuta ya kupakaa na mengineyo)
x. Tochi moja ndogo kwa matumizi ya mwanafunzi usiku.
xi. Sare ya bweni gauni la pinki mshono wa soro na wavulana track suti nyeusi
xii. Vifaa vya usafi jembe lenye mpini
xiii. Kandambili za kuogea.

## B. WANAFUNZI WA KUTWA

i. Fedha Tsh:90,000/=(Elfu tisini)
ii. Mahindi debe tano (5) kwa mwaka
iii. Maharage debe moja (1) kwa mwaka
iv. Mchele lita kumi (10) kwa mwaka
v. Sukari kilo nne (4) kwa mwaka
vi. Sahani, kijiko na kikombe.
vii. Vifaa vya usafi panga na fyekeo.

**NB: MALIPO YOYOTE YA FEDHA YAFANYIKE BENKI YA NMB KWENYE AKAUNTI NAMBA AC60306600125 JINA LA AKAUNTI NI DEVELOPMENT ACCOUNT.**

**SHULE YA SEKONDARI ILEMBULA, S.L.P. 33, ILEMBULA.**

**SHERIA ZA SHULE.**

**SEHEMU A: MAMBO YAMPASAYO MWANAFUNZI AYATEKELEZE KIKAMILIFU (DO's)**

1. Kufuata vyema ratiba ya shule kwa kuamka mapema na kukimbia mchakamchaka, kufanya usafi binafsi na wa mazingira ya shule, kuhudhuria mihadhara ya kawaida nay a dharura, kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ya darasani, kushiriki shughuli nyinginezo za shule baada ya vipindi vya darasani, kushiriki sara za jioni na kuhudhuria maandalio ya jioni (evening preparation). Thamani muda kwa kila jambo lililopo kwenye ratiba.
2. Kuwa mfano bora wa heshima na tabia njema popote alipo. Hii ni pamoja na kusalimia kwa heshima, kuwaheshimu watu wote (walimu, wafanyakazi wasio walimu, wazazi/ walezi, viongozi mbalimbali wa dini na serikali za wanafunzi wenzako) na kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, wimbo wa taifa, Nembo ya Taifa na fedha ya Taifa.
3. Kukaa kimya muda wote awapo darasani na kutoka nje bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa lake.
4. Kuvaa sare husika na iliyoruhusiwa wakati wowote mwanafunzi awapo ndani na n je ya shule. Wakati wa safari kuja shule au kurudi nyumbani wakati wa likizo ni lazima kuva sare ya shule na kitambulisho cha shule. Wakati wa michezo vaa sare za michezo, wakati wa kazi za mikono vaa sare za kazi na wakati wa darasani vaa sare ya darasani. Kofia au mapambo yoyote si sehemu ya sare za shule.
5. Kuwahi kurudi shuleni kwa tarehe iliyopangwa kufungua shule. Wachelewaji watachukuliwa hatua sambamba na kuletwa na wazazi/ walezi wao vingnevyo hatapokelewa shuleni kuendelea na masomo akija peke yake.
6. Kuitika kwa haraka wito wa dharura na wakawaida na kukimbilia aliko mtu anayekuita au unapotakiwa kukusanyika. Hii ni pamoja na kutoa taarifa ya viashiria vyovyote vya uvunjifu wa amani na hatarishi la usalama wa wanafunzi na mali zao na mali za shule.
7. Kusimama katika mistari wakati wa kupokea huduma mbalimbali yakiwemo matangazo, chakula au vifaa vya kazi.
8. Kunyoosha mkono unapouliza au kujibu maswali.
9. Kuzingatia usafi wa mwili, mavazi, mabweni, madarasa na mazingira yote ya shule. Kila mmoja ashiriki mahali alipopangiwa kufanya usafi na kuzingatia usafi binafsi
10. Utunzaji na utumiaji mzuri wa mali za shule zitumiwazo kwa shughuli za shule mabwenini,ukumbini, madarasani, ofisini na mahali pengine. Mali binafsi za wanafunzi wenzako vithaminiwe nakutunzwa. Uharibifu wowote wa mali za shule au binafsi lazima ufidiwe na aliyeharibu.
11. Kuwasiliana na wazazi/ walezi kwa kutumia simu ya matroni aliyeteuliwa kwa kazi hiyo

**SEHEMU B: MAKATAZO MAKUU KWA MWANAFUNZI (DON'Ts)**

1. Kutotumia lugha mbaya kwa walimu, wazazi/ walezi, wafanyakazi wasio walimu,wanafunzi wenzake na jumuiya nyingine nje ya shule.
2. Kutotumia madawa ya kulevya ya aina zote wala kuvuta sigara.
3. Kutokumbatia uchafu kwa kufuga kucha ndefu, nywele ndefu, ndevu na kuvaa mavazi yasiyo ya heshima hii ni moja ya kushona sare kwa kuzingatia maelekezo ya kujiunga na shule (mfano: **suruali za kubana au gauni fupi kwa wasichana)**
4. Kututoka nje ya mipaka bila kibali cha mamlaka ya shule.
5. Kutotembelea nyumba za wafanyakazi wa shule , vilabu vya pombe na baa, majumba ya starehe na nyumba za kufikia wageni ( guest house).
6. Kutofanya maongezi yoyote na Mzazi/ Mlezi bila kibali cha mamlaka ya shule na katika siku zisizo ruhusiwa. Hii ni pamoja na kutotumia maeneo ya nyumba za ibada kama sehemu za wazazi/ walezi kuonana na wanafunzi, kuongea nao na kuwapa baadhi ya vyakula visivyoruhusiwa kwa mwanafunzi.
7. Kutokiuka maelekezo 1-11 ya sehemu A hapo juu kwani kufanya hivyo ni kosa linalostahili adhabu.

**FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI KUTII SHERIA ZA SHULE NA KUTOSHIRIKI FUJO, MIGOMO NA MAKOSA YA JINAI**

***(Ijazwe kikamilifu na mwanafunzi na Mzazi/Mlezi na kuhifadhiwa kwenye faili binafsi la mwanafunzi shuleni)***

Mimi………………………………………… wa kidato cha ……………..mwaka 20….. ninakiri kuwa nimeelimishwa na kuzielewa sheria za shule kama zilivyoletwa na Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi Stadi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuletwa shuleni kuiongoza Jumuiya ya shule ya sekondari Ilembula ambayo mimi ni mmoja wao. Naahidi utii wa sheria hizi bila shuruti na kwamba ni hatia kwangu kuzikiuka sheria hizi ninastahili na nitapokea adhabu kwa mujibu wa sharia hizo .

Sahihi ya mwanafunzi: ………………………………………………. tarehe:……………………

**FOMU YA AHADI YA MZAZI/ MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE NA MAELEKEZO MENGINE YALIYOTOLEWA KWA MTOTO WAKE.**

Mimi …………………………… ambaye ni mzazi/ mlezi wa mwanafunzi ……………………………….

Wa kidato cha …………….. mwaka……… ninakiri kuwa

Nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na maelezo ya kujiunga na shule ikiwa ni pamoja na kanuni za shule. Nina kubaliana na mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari Ilembula kuanzia tarehe……………… naahidi kutoa ushirikiano na uongozi wa shule ili kuhakikisha mwanafunzi mtajwa hapo juu anafuata sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule bila usumbufu wowote. Nitakua tayari kumpokea mtoto wangu wakati wowote endapo atakiuka sharia na hivyo kufukuzwa shule.

Sahihi ya Mzazi/ Mlezi…………………………………………………Tarehe:……………………..

**SHULE YA SEKONDARI ILEMBULA, S.L.P.33, ILEMBULA.**
**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

A. 1. Jina la mwanafunzi……………………………………………….
   2. Tarehe ya kuzaliwa…………… Mwezi …………… Mwaka ……………..
   3. Mahali alipozaliwa kijiji……………………………Kata ya……………………
      Wilaya…………………………….. Mkoa……………………………..
   4. Dini……………………………… Dhehebu……………………………………..

B. 1. Jina la Mzazi/ Mlezi ………………………………………………..
   2. Kazi ya Mzazi/ Mlezi ………………………………………………..
   3. Anwani ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………..
   4. Mahali anapoishi Mzazi/ Mlezi………………………………………

C. Majina ya ndugu wengine wanaohusika na malezi ya mwanafunzi huyu.
   1. Jina la ndgu……………………………………………………………
   2. Mahali anapoishi, kijiji……………………………. Kata ya………………………….
      Wilaya ……………………….. Mkoa………………………Namba ya simu……………………

D. Taarifa za viongozi wa ofisi ambako Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi anaishi.
   1. Jina la afisa mtendaji wa kata (WEO)……………………………………………………….
      Kata ya ……………………………… S.L.P……………………………
   2. Jina la mwenyekiti wa kijij ………………………………………………
      Kijiji cha…………………………S.L.P………………………………..
      Sahihi na mhuri ………………………………………. Namba ya Simu………………………..

ILEMBULA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 33,
ILEMBULA.
Date……………………………

**To the medical officer**
…………………………………
…………………………………

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

(To be filled by district/regional medical officer and brought to the school by the student in his/her first arrival)

Student's full name………………………………sex………………………age………

Please examine the above named student as to his / her fitness for full secondary education course

**………………………………**

**HEAD OF SCHOOL**

Blood count (Red and White)……………………………………………..........................
Stool examination……………………………………………………………………....
Urine analysis……………………………………………………………………………
Syphilis test………………………………………………………………………………
Eye test……………………………………………………………………………………
TB test……………………………………………………………………………………
Ears………………………………………………………………………………………
Chest………………………………………………………………………………………
Spleen……………………………………………………………………………………
Abdomen…………………………………………………………………………………
Blood pressure……………………………………………………………………………
Pregnancy test…………………………………………………………………………....

**ADDITIOANAL INFORMATION (if any) eg. Physical**

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………….................................

**MEDICAL CERTIFICATE**

(to be filled by the examining medical officer)

I certify that the above mentioned student is fit/not fit for full secondary education course

Name……………………………………………………signature……………………….
Designation…………………………………………….date………………………….
Official rubber stamp……………………………

**NOTE**: Medical officer should report any important noticed at the time of examination of the individual, you must bring this completed form when you come to school. No any student may be without certificate of medical examination.